

Nini unapaswa kujua kuhusu Programu za Umma

1. Wakimbizi na wenyeukimbizi wunaweza kupata msaada kutoka SSI, TANF, misaada ya chakula na faida kamili kutoka MaineCare. Hii ina maana kwamba kama umeomba ukimbizi na unasubiria maamuzi, mara utakapo pata hadhi ya ukimbizi utakubalika kwenye program hizi.

2. Bila kujali hali yako ya uhamiaji kama uko nchini Marekani kihalali unaweza kupata :

- **Msaada wa Jumla** kutoka mji wako au mji;
- **SSI** itasaidia kulipa mahitaji ya msingi kama una umri wa zaidi miaka 65 au kama una ulemavu;
- Faida ya **MaineCare** kama ni mjamzito au chini ya miaka 21, na

3. Katika baadhi ya familia, baadhi ya watu wanaweza kupata msaada kutoka kwa programu za umma wakati wengine hawawezi. Kwa mfano, mama anaweza asiwe na hadhi ya kupata MaineCare lakini watoto wake wakastahili. Hii ina maana kwamba unahitaji kufikiria kama mtu yeyote katika familia yako anakubaliwa.

4. Huna haja ya kuonyesha ushahidi wa hali yako ya uhamiaji kama unaomba msaada kwa ajili ya jamaa wa familia yako na sio wewe.

- Kama unaomba kwa ajili ya familia , unapaswa kuwaambia/kumuambia mfanyakazi wa DHHS kwamba maombi hayahusiani na wewe.
- Kama umesema haya, na mfanyakazi wa kesi anauliza kuhusu ushahidi wa hali yako ya uhamiaji, unaweza kusema **HAPANA.**

5. Sheria inasema kwamba kama mtoto anakubalika kupata msaada, mtoto anatakiwa asaidiwe hata kama hautojibu swali kuhusu hali yako ya uhamiaji.

6. Kama hauna nyaraka za ukaaji kihalali unaweza kupata msaada katika program zifuatazo:

- Msaada wa Matibabu ya Dharura;
- WIC (chakula kwa ajili ya wanawake wajawazito na watoto);
- Chakula cha mchana shuleni.
- Kinga, upimaji na tiba ya dalili za magonjwa ya kuambukiza;
- Head Start; na

- Makazi kwa wasio na malazi na waathirika wa ukatili wa majumbani. .

Kwa maswali wasiliana na:

Maine Equal Justice Partners	Immigrant Legal Advocacy Project (ILAP)
207-626-7058 au piga bure katika 1-866-626-7059	207-780-1593 au piga bure katika 1-800-497-8505
www.mejp.org	www.ilapmaine.org